JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

TAMKO LA MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.) WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO, NA TEKNOLOJIA YA HABARI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA MAADHIMISHO YA 44 YA SIKU YA POSTA AFRIKA TAREHE 18 JANUARI, 2024

Kauli Mbiu: "Kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Wateja Wenye Ufanisi"

Katika kuadhimisha Siku ya Posta Afrika, Umoja wa Posta Afrika umekuwa kiungo muhimu cha maadhimisho haya ambayo huadhimishwa kila mwaka Barani Afrika.

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kutoa shukrani za dhati na pongezi kwa Umoja wa Posta Afrika (PAPU) kwa kufikia hatua hii muhimu. Maadhimisho ya mwaka huu ni ya kipekee kutokana na uwepo wa enzi hizi za kidijitali ambazo zimeleta mabadiliko makubwa katika uchumi wa Bara la Afrika.

Uwepo wa PAPU umekuwa muhimu katika kuchochea mawasiliano Kikanda, kuinua viwango vya mawasiliano, na kuchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya huduma za posta katika Bara la Afrika. Azma ya umoja ni kufikia malengo yake ya kutambuliwa na kuthaminiwa.

Tukiangazia mafanikio ya PAPU tangu kuanzishwa kwake, tunatambua jukumu lake muhimu katika kuchochea mabadiliko ya haraka katika Sekta ya Posta na kuendana na enzi za kidijitali zilizopo sasa. Kumbukumbu hii inapaswa kuwa ni ushuhuda wa athari chanya na endelevu ya umoja huu katika kutoa huduma bora katika Sekta ya Posta Barani Afrika.

Leo, tunasherehekea si tu mafanikio yaliyofikiwa bali pia fursa ya ubunifu, ufanisi na ukuaji endelevu wa siku zijazo. PAPU imechangia kwa kiasi kikubwa katika kuweka mazingira wezeshi, kubadilisha uzoefu katika Sekta miongoni mwa wadau wa posta pamoja na kutatua changamoto za pamoja zinazokabili Sekta ya Posta katika nchi za Afrika. Juhudi hizi za ushirikiano wa PAPU sio tu zimeimarisha Sekta ya Posta bali zimeongeza mchangamano wa Kikanda pamoja na kuchochea ukuaji wa kiuchumi.

Kauli mbiu ya mwaka huu inayosema "Kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Wateja Wenye Ufanisi" inaashiria juhudi za dhati ndani ya Umoja wa Posta Afrika katika kuboresha na kufikia kiwango wezeshi cha utoaji wa huduma kwa wateja.. Uchaguzi wa kauli mbiu hii unathibitisha ahadi ya kuweka mazingira wezeshi ya kuchangamana na wateja ambayo yanapelekea uimarishaji wa mawasiliano, Sera na Kanuni zinazoendana na mazingira husika, kushughulikia kwa ufanisi masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Posta na hatimaye kuleta uzoefu chanya na bora kwa watumiaji wa huduma za posta.

Ufanisi katika Mifumo yetu ya Usimamizi wa wateja sio wa kinadharia bali ni lazima kwa ukuaji na umuhimu wa Sekta yetu ya Posta. Katika ulimwengu ambapo mawasiliano yanakua kwa haraka, dhamira yetu ya kuimarisha uvumbuzi ni muhimu ili kuhakikisha kwamba nchi wanachama wa PAPU, zinaendelea kuwa mstari wa mbele katika kutoa huduma bora za posta.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na dhamira yake ya kuboresha, kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za posta zenye, kuaminika, na zenye gharama nafuu nchini . Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 kwasasa inafanyiwa maboresho ili kuendana na Mfumo wa kitaasisi unaojumuisha Serikali, Mdhibiti, Watoa Huduma za Posta na Wateja.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inadhibiti na kufuatilia maendeleo katika Sekta ya Mawasiliano, ambayo Sekta ya Posta ni sehemu yake. Kwa upande mwingine, Shirika la Posta Tanzania (TPC) na watoa huduma wengine wa usafirishaji kutoka Sekta binafsi wana jukumu la kutoa huduma za posta ndani na nje ya nchi kupitia mtandao wa posta wa kitaifa na kimataifa, ambao unawapa wateja uwanja mpana wa kutumia huduma za posta.

Vilevile, katika kuboresha Sekta ya Posta kuwa ya kidijitali, Tanzania ina Sera ya TEHAMA pamoja na Sera ya Taifa ya Posta inayofanyiwa mapitio ambazo kwa pamoja zinalenga kukuza huduma za posta. Katika kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Wateja wenye Ufanisi, Shirika la Posta linatumia mfumo wa kufuatilia mwenendo wa barua au vifurushi vya haraka pamoja na rejista ndani na nje ya nchi. Aidha, Shirika la Posta Tanzania hutumia kikoa cha .post kwenye Duka la Posta, ambalo ni salama na la kuaminika katika mazingira ya uchumi wa kidijitali.

Kauli mbiu inatuambia kwamba Sekta ya Posta imekuwa uti wa mgongo wa mawasiliano na biashara, na inaendana na mabadiliko makubwa ya kidijitali ambayo yanaongeza ufanisi na usimamizi wa wateja. Leo, hatuadhimishi kuhusu barua na vifurushi bali pia kuhusu kubadilishana habari za kidijitali katika Sekta ya Posta, huduma za malipo, huduma za serikali za mtandao, afya mtandao, kilimo mtandao, biashara mtandao na kujenga uhusiano. Katika hali hii ya mabadiliko ushirikiano umekuwa msingi wa mustakabali wetu sasa na baadaye.

Tunapoadhimisha Siku ya Posta Afrika, Tanzania inatambua umuhimu wa mfumo wa usimamizi wa wateja wenye ufanisi katika kuhifadhi taarifa za wateja, kumbukumbu za wateja, kuwezesha mahitaji ya wateja, kuboresha mawasiliano na wateja, kutoa uamuzi kwa kutumia taarifa za wateja, ukuaji wa Sekta, na kuzitangaza huduma za posta nchini.

Siku ya Umoja wa Posta Afrika mwaka 2024 inatumika kama llani kuifikia dhamira yetu ya kuhakikisha huduma za posta zinawafikia na kuvuka matarajio ya wateja. Tukiongozwa na kauli mbiu ya mwaka huu, tunaanza safari kuelekea ufanisi mkubwa katika kuwahudumia wateja jambo litakalopelekea kumbukumbu ya kudumu katika umoja wetu. Ni muhimu kusisitiza kwamba mwelekeo wa baadaye wa Sekta ya Posta unategemea uwezo wake wa kubuni na kuwezesha biashara za posta kuleta suluhisho la mawasiliano.

Kwa niaba ya Serikali, nawahakikishia ushirikiano endelevu katika jitihada za kuhakikisha Sekta ya Posta inakuwa ya kisasa na ya kuaminika nchini Tanzania. Pamoja, tunajenga mustakabali wa baadaye ambapo kila kifurushi, barua, na mawasiliano ya posta yanajikita katika ufanisi na maendeleo ya Sekta ya Posta. Hongera tena kwa tukio hili kubwa, na tuendelee kushuhudia mafanikio na maendeleo ya Umoja wa Posta Barani Afrika katika huduma za posta.

Nawatakia heri na mafanikio katika kuadhimisha Siku ya Posta Barani Afrika huku tukitaraiia mafanikio zaidi katika siku za karibuni



TANZANIA COMMUNICATIONS REGULATORY AUTHORITY (TCRA)

TAARIFA YA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA) DKT. JABIRI K. BAKARI KATIKA MAADHIMISHO YA 44 YA SIKU YA POSTA AFRIKA - 18 JANUARI 2024

TCRA Director General, Dr. Jabiri K. Bakari

Kauli mbiu "Kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Wateja Wenye Ufanisi".

Leo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaungana na Umoja wa Posta Afrika (PAPU) kuadhimisha miaka 44 ya Siku ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU). Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), napenda kuchukua fursa hii kuipongeza sekta ya Posta barani Afrika na Sekretarieti ya Umoja wa Posta Afrika, yenye makao yake makuu Arusha, Tanzania, katika maadhimisho haya maalum.

Tunapoadhimisha Siku ya PAPU, ni wakati wa kutafakari juu ya kujitoa kwetu kuhakikisha ubora na uvumbuzi katika huduma za Posta. Huu ni wakati muhimu kwa Mamlaka ya Mawasiliano kama mdhibiti wa posta kuendelea kutetea na kukuza ufanisi na ubora katika shughuli za posta kwa kuhakikisha kuna mazingira mazuri ya udhibiti.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni *"Kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Wateja Wenye Ufanisi".* Mada hii inasisitiza umuhimu wa kutekeleza mfumo ulioboreshwa na madhubuti wa kudhibiti mwingiliano wa wateja ndani ya sekta ya posta. Lengo ni kuhakikisha kuwa, mifumo ya watoa huduma za Posta inakidhi mahitaji ya wateja wao, inachangia kuboresha mahusiano ya wateja nchini na nchi nyingine za Afrika ili kuwezesha kufanyika kwa biashara zaa mipakani. Ni muhimu kwa watoa huduma kukidhi mahitaji mbalimbali ya wateja na kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia katika mawasiliano ya posta.

Zaidi ya hayo, kwa kutambua uwepo wa mabadiliko ya uvumbuzi katika kiteknolojia unaendelea kwa kasi katika sekta zote ikiwa ni pamoja na sekta ya posta nchini, baadhi ya ubunifu unaohusisha sekta ya posta huenda matumizi ya vitendo usionekane kwa sasa au unaweza kuhitaji muda kukomaa huku nyingine zikiwa na uwezo mkubwa wa kuvuruga hali ya biashara iliyopo au huduma kwa wateja kwa sasa au katika siku za usoni. Kuendelea na juhudi za kupunguza changamoto ambazo bado zinaathiri uwezo wa Huduma ya Posta wa kutekeleza teknolojia kutakuwa ufunguo wa kufikiwa kwa malengo ya uvumbuzi. Kwa hiyo, kuwahudumia wateja vyema zaidi kwa kutumia ubunifu wa TEHAMA ambao unanea kupitia mfumo wa kijamii ambao unaleta athari chanya kwa wateja kuridhia ubora wa huduma zitolewazo unatokana na kuboresha mazingira ya huduma, utoaji wa huduma na michakato mingine.

TCRA kwa kushirikiana na wadau wengine wa sekta wanajitahidi kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara mtandaoni katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Kubadilisha ofisi za posta kote Tanzania ili kutoa huduma za umma sehemu moja kutafanya lengo la hili kufanikiwa kwa haraka. Katika maadhimisho ya mwaka huu ya kuadhimisha miaka 44 ya PAPU, Tanzania ina imani kuwa ubadilishanaji wa bidhaa na huduma za posta kuvuka mipaka na upatikanaji wake kupitia mitandao ya kitaifa ya sekta ya Posta utakuwa wa kweli ndani ya kipindi kilichokusudiwa na azimio la Umoja wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Kidijitali kwa Afrika. 2020-2030).

Sekta ya Posta inabaki kuwa sekta muhimu sana kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya taifa letu. Kama sisi sote tunajua kwamba maendeleo ya TEHAMA yamebadilisha biashara ya posta ya jadi na kuunda njia ya huduma mpya za posta za TEHAMA. Ujio wa wa biasharamtandao na huduma zingine za kielektroniki ulipokelewa vyema na watoa huduma za posta duniani kote, na kwamba mtandao wa posta unatumika kama njia ya kuaminika ya utumaji na upokeaji wa wa bidhaa zilizoagizwa kupitia biasharamtandao.

Kama sehemu ya mkakati wa kuhakikisha kuwa wateja wanapata huduma ya posta yenye bei nafuu na inayotegemewa, TCRA imetoa leseni kwa Shirika la Posta Tanzania na watoahuduma wengine wa kusafirisha vifurushi na Nyaraka 116 ambao wamewekwa katika makundi atika makundi matano (5) ambayo ni; Watoa huduma za Kimataifa (International Courier Operator)– 6, Watoa huduma wa Afrika Mashariki (East Africa Courier Operator)– 1, Watoa huduma ndani ya mipaka ya Tanzania (Domestic Courier Operator) – 45, Watoa huduma katika mji mmoja (Intra-city Courier Operator) –14 na Watoa huduma wanaotumia mabasi ya Abiria (Inter-city Transporter Courier Operator)– 50 kwa kipindi cha Desemba, 2023. Wenye leseni hawa na wengine wanapata huduma wanatumia huduma za udhibiti na lesni zao mtandaoni kupitia mfumo wa leseni wa TANZANITE.

Ninapohitimisha taarifa yangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzindua na kukabidhi jengo la Makao Makuu ya PAPU (PAPU TOWER) tarehe 2 Septemba, 2023. Uzinduzi wa Jengo hili la PAPU utaendelea kuwa chachu ya kuendeleza sekta ya posta na kukuza ushirikiano zaidi na Wadau wa Posta duniani kwa kuwa na kituo cha ubora na kutengeneza nafasi nyingi za ajira kwa Watanzania.

Kwa mara nyingine tena, kwa niaba ya Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa TCRA ninawatakia nyote Heri ya Mwaka Mpya 2024 tunapoadhimisha miaka 44 ya PAPU.

DKT. JABIRI K. BAKARI
MKURUGENZI MKUU, MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)
Jumatano, 18 January 2024

KUTOKA DAWATI LA POSTAMASTA MKUU WA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA

KATIKA KUADHIMISHA KUMBUKUMBU YA KUANZISHWA KWA UMOJA WA POSTA AFRIKA(PAU) 18 JANUARI, 2024

Maharage A. Chande Postamasta Mkuu

Kauli Mbiu: **"Kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Wateja Wenye Ufanisi"**

Tarehe 18 Januari kila mwaka, Shirika la Posta la Tanzania (TPC) linajumuika na wadau wengine wa posta barani Africa kusherehekea Maadhimisho ya kuanzishwa kwa Umoja wa Posta wa Afrika (PAPU), Umoja wa Kikanda wenye Makao Makuu yake jijini Arusha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Umoja huu ulianzishwa tarehe 18 Januari 1980 katika Mkutano wa Mkuu wa Mawaziri wenye dhamana ya Posta, wakati huo ikiwa ni chini ya Umoja wa Afrika ukijulikana kama Shirikisho la Umoja wa Afrika (OAU).

PAPU ni Umoja wa Posta za Kiafrika, taasisi hii inashughulikia maendeleo ya huduma za posta kupitia waendeshaji na watoa huduma za Posta Barani Afrika. Kauli mbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu ni "Kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Wateja Wenye Ufanisi," inaakisi uhalisia, ikisisitiza jukumu muhimu la kuridhika kwa wateja, imani, na maendeleo ya teknolojia katika taswira inayobadilika ya huduka za posta, huku tukizingatia jukumu la posta katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi.

Siku ya Umoja wa Posta Afrika ni kumbukumbu inayogusa chimbuko la ushirikiano na uthabiti uliojitokeza kwenye mtandao wa posta, kurahisisha mawasiliano, biashara, na mabadilishano ya kitamaduni katika ardhi zetu tofauti kwa vizazi.

Siku ya leo si tu kusherehekea mafanikio tuliyopata bali pia kutambua changamoto na fursa zilizo mbele yetu kama sekta. Kauli mbiu hii ya 2024, "Kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Wateja Wenye Ufanisi," inaendana kikamilifu na azma yetu kama Shirika la Posta la Tanzania na kwa nchi kwa ujumla. Tukitambua kuwa mfumo imara wa usimamizi wa wateja ni muhimu kwa kuboresha kuridhika kwa wateja na kuaminika, hasa katika zama hizi za maendeleo ya haraka ya teknolojia. Tukijenga Tanzania ya kidijitali, tunalenga kumtumikia mteja mteja wetu aridhike.

Umoja wa Posta Afrika inafanya juhudi ili kuimarisha ushirikiano kwa watoa huduma za Posta barani Afrika, ikiwa na ahadi ya kukuza ushirikiano, kuwekeza katika uvumbuzi, na kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika kuhakikisha tunatoa huduma za kisasa zaidi. Mazingira ya kisasa yanatoa fursa nyingi za biashara mtandaoni pamoja na huduma za kifedha za kidijitali, ambazo watoa huduma za posta wanajitahidi kuzitumia kuboresha huduma kwa wateja.

Katika kuendana na taswira inayobadilika ya tasnia ya posta, kwetu Shirika la Posta la Tanzania, tunathamini na kutambua mchango wa kila mfanyakazi katika kulipeleka Shirika letu kwenye mafanikio mapya. Tunaelewa kwamba wateja wetu ni nguzo muhimu ya biashara zetu za posta, na kukidhi mahitaji ya wateja ni muhimu, hivyo tunaupa kipaumbele mwelekeo wa kumzingatia mteja na kuzidisha matarajio ili kukuza uaminifu na uzoefu chanya kwake. Na katika kutekeleza hilo tumeanzisha duka la mtandaoni la posta (https://www.postashoptz.post/) na lile la stempu e-philately (https://stamps.tz.post/) ambapo wateja wetu wa thamani wanaweza kufikia huduma zetu mtandaoni bila usumbufu wowote.

Shirika letu linaelewa kuwa, dunia inaendelea kubadilika na hivyo ni lazima tuendane na mabadiliko hayo, wakati tunakumbatia maendeleo ya teknolojia kwa kubadili mifumo yetu ya utoaji huduma iwe ya kidigitali zaidi, vilevilé si tu kwa kubadili mifumo lakini pia kuwa mstari wa mbele katika kuwaendeleza wafanyakazi katika kukidhi mahitaji ya wateja wetu kwa kutumia teknolojia.

Kwa muktadha huu, tunapoadhimisha maendeleo ya huduma za posta barani Afrika, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wa posta wanaojitolea kote Afrika, ikiwa ni pamoja na timu yetu katika Shirika la Posta la Tanzania, kwa azma yao isiyoshindwa, hasa katika kipindi cha chenye changamoto nyingi, inajenga misingi ya utoaji wa huduma bora, azma na uthabiti unaofanana si tu mtazamo wa timu ya posta za Kiafrika bali pia mtazamo posta kimataifa.

Tunapoadhimisha Siku ya kuanzishwa kwa PAPU miaka 44 iliyopita, Shirika linapenda kuhamasisha na kuwahimiza wateja wetu wa wapendwa na wa thamani kuendelea kufurahia huduma zetu za kisasa zaidi zinazopatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu kukidhi mahitaji yao ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nimalizie kwa kuwatakia nyote maadhimisho mema ya Siku ya PAPU!

Maharage A. Chande
Postamasta Mkuu